# SALA CHAKULANI

UTANGULIZI

1. Wakristo wakiwa pamoja au pekepeke kila wanapoketi chakulani na wanapomaliza kula huwa wanamshukuru Mungu ambaye kwa maongozi yake amewajalia riziki ya siku hiyo kama walivyomuomba katika sala ya Baba Yetu.
Hasa wanatakiwa kukumbuka kwamba Bwana Yesu alipenda kuunganisha sakramenti ya Mwili na Damu yake na tendo la kula karamu, na kwamba kisha kufufuka katika wafu alijitambulisha kwa wanafunzi wake katika kuwamegea mkate.

2. Wakikaribia meza iliyoandaliwa chakula, wanachokitambua kuwa ni ishara ya baraka ya Bwana kwao, hawatakiwi kuwasahau mafukara ambao pengine wanapata sehemu ndogo tu ya chakula wanachohitaji.
Kwa hiyo wajitahidi iwezekanavyo kujinyima ili wawasaidie; pengine watekeleze maneno ya Kristo (Lk. 14:13-14) kwa kuwakaribisha mezani pao kama ishara ya udugu.

3. Matini ya kijitabu hiki lengo lake ni kusaidia tu familia na jumuia mbalimbali zifaidike kiroho na tendo la kujipatia mahitaji ya mwili, kwa kusali kadiri ya vipindi vya mwaka wa liturujia na kufuatana na Kitabu cha Baraka cha Kanisa Katoliki la Kilatini (toleo la mwaka 1984).
Baraka zinashika nafasi muhimu kati ya visakramenti vilivyowekwa na Kanisa kwa faida ya waamini: kwa ibada hizo taifa la Mungu linamsifu yeye na kujiandaa kupokea neema za sakramenti na kutakasa nafasi mbalimbali za maisha, kama hiyo ya kula.

4. Mbali na ibada za kuanzia na kumalizia, mpangilio wa kawaida wa baraka za chakula una sehemu mbili: kwanza tangazo la Neno la Mungu, halafu sifa ya wema wake pamoja na ombi la msaada wake.
Vitendo mbalimbali vinaweza vikaendana na maneno ya sala (hasa ikiongozwa na askofu, padri au shemasi), kama vile kufanya ishara ya msalaba na kunyosha, kuinua au kufunga mikono.
Inaongezwa namna nyingine fupi zaidi kwa siku yoyote, inayofaa hasa kukaririwa na kutumiwa pasipo kijitabu hiki.

5. Baada ya chakula mpangilio wa kawaida una sala ambayo inafaa itanguliwe na wimbo wa antifona.

# KABLA YA KULA

## KAWAIDA - I

Kiongozi anasema:

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.**

Wote wanaitikia:

**Amina.**

Mmojawapo anatangaza somo fupi kutoka Maandiko Matakatifu linalohusu tendo la kula au tukio lingine la maisha ya wahusika, au liturujia ya siku.

Hatimaye kiongozi anawaalika wote wasali kidogo kabla hajatoa sala rasmi:

**Tuombe.**

Baada ya nafasi ya kimya, kiongozi anamalizia kwa kusema**:**

**Wema wako hauna mwisho, Baba!**
**Utujalie sasa ukarimu na uhuru wa moyo**
**tuweze kujitoa mhanga kwa ndugu zetu**
**kama punje ya ngano ambayo ikifa inazaa sana,**
**au kama chakula hiki ambacho kikiliwa**
**kinatuongezea nguvu na uzima.**
**Tunakuomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

Wote wanaitikia:

**Amina.**

## KAWAIDA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu, mahali pote ulimwenguni wewe upo,**
**hasa ndani yetu binadamu tulio mfano wako:**
**utubariki sasa pamoja na chakula chetu,**
**tupate kuendelea safari yetu kwa upendo wako.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Utukuzwe, ee Bwana Mungu wa ulimwengu**
**kwa alama hizi za wema wako**
**tunazotaka kuzipokea kwa shukrani:**
**uzibariki na kuwajalia mataifa yote pia**
**wafurahie maongozi yako ya ajabu.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - IV

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Ee Bwana, unayedumisha viumbe vyote,**
**huwanyimi riziki watoto wako:**
**sote pamoja tunakusifu kwa maisha unayotujalia**
**na kwa chakula hiki cha kututia nguvu mpya;**
**tena tunakuomba kwa neno lako**
**utegemeze imani yetu pia**
**tukatafute hasa ufalme wako.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - V

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Ee Mungu mpenda uzima,**
**tunakusifu kwa viumbe vyako vyote**
**na kwa chakula chetu hiki unachotujalia.**
**Wewe unayelisha ndege wa angani**
**na kuvika maua ya porini,**
**usikubali mtu yeyote akose riziki zake.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - VI

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mungu wa rehema zote,**
**wewe unaimarisha umoja wa watoto wako**
**unapowaalika wale chakula pamoja;**
**utubariki hata leo sisi na neema hizi**
**tupate kushirikiana kwa furaha na unyofu wa moyo**
**na kustawisha upendo wetu wa kidugu.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - VII

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu, Mchungaji wa milele,**
**kweli unatulisha wanao kwa upendo wa Kibaba:**
**kwa kubariki sasa zawadi zako hizi**
**utujalie moyo wa shukrani kwako wewe**
**na kwa wote wanaotusaidia.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - VIII

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Huruma yako, Baba, haina mipaka!**
**Kwa kazi zetu unatujalia chakula cha kila siku**
**na vilevile tuzo la milele;**
**basi, tunakusifu na kukuomba sana:**
**vitu hivi ambavyo tutashirikiana katika upendo wako**
**vituburudishe na kutupa nguvu**
**tuendelee kufanya kazi hizo**
**kwa furaha na bidii nyingi zaidi.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - IX

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Tunakutumainia bila ya wasiwasi, ee Mungu,**
**uliyeumba na kudumisha vyote kwa upendo mkuu:**
**tunakusifu kwa neema ulizotuandalia mezani hapa,**
**tena tunakuomba tuwe imara katika imani**
**hata kwenye matatizo ya maishani,**
**na kuwashirikisha ndugu zetu wote**
**furaha ya kuwa watoto wako na warithi wa mbinguni.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

MAJILIO - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba, huruma zako ni nyingi sana:**
**ulimtuma kwetu Mwanao wa pekee**
**tupate kuwa na uzima, uzima ulio kamili.**
**Utujalie sasa nguvu mpya kwa chakula hiki**
**tukae macho mpaka Bwana Yesu atakaporudi mtukufu.**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

MAJILIO - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mungu, Baba wa huruma,**
**ulipanga Mwanao avae ubinadamu wetu:**
**utubariki sisi na zawadi zako hizi,**
**na kutujalia tumngojee kwa moyo wazi na motomoto**
**yeye, anayeishi na kutawala daima na milele.**

MAJILIO - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba, sifa zetu zipande kwako,**
**huku baraka yako ikishuka juu ya chakula hiki**
**kitakachotutegemeza safarini**
**tunapoelekea kukutana na Mwanao.**
**Wakati huu tunapomngojea**
**uwashe hasa ndani mwetu**
**hamu ya kukupata wewe na ufalme wako.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

NOELI - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Shukrani kwako, Mungu wa upendo,**
**uliyetunukia tumaini la maskini**
**kwa uzazi wa Bikira Maria.**
**Tafadhali sana: utujalie imani kama ya kwake**
**tukampokee Mwanao katika kila mtu**
**na kumshirikisha kidugu chakula chetu.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

NOELI - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba, kwa Mwanao kuzaliwa na Bikira Maria**
**umeonyesha jinsi gani unavyowapenda watu.**
**Sasa kwa kutubariki sisi na chakula hiki**
**utuweke tayari kuwahudumia kwa upendo ndugu wote.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

KWARESIMA - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba yetu mpole,**
**waliotubu unawasamehe kabisa**
**na kuwapokea kwa furaha;**
**basi ubariki chakula hiki**
**tulichopata kwa jasho la uso,**
**tena utujalie roho zetu ziongoke**
**hata tustahili kukubaliwa nawe.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KWARESIMA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Tunakusifu, Bwana, kwa kutulisha
mkate wako na neno lako.
Tunakuomba pia: mafukara wote duniani
waketi mezani pako
tukashiriki pamoja nao
katika karamu ya ufalme wako.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KWARESIMA - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu, Baba yetu,
katika ulimwengu huu usio na amani
ulimtuma Mwanao usimuepushe na kifo
ili turudishiwe uzima wako;
basi, uzibariki neema hizi
na kutugeuzia uchungu wa makosa yetu
uwe furaha ya kusamehewa nawe.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KWARESIMA - IV (NA SIKU ZA MFUNGO)

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba mwenye huruma, Mungu unayetuchunga,
kwa neema yako tumeamua chakula chetu leo
kiwe kidogo kuliko kawaida
ili wenzetu wapate kula zaidi:
uyazidishe matunda ya kujinyima kwetu
kwa faida ya mafukara na wenye shida yoyote.
Tunakuomba kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## JUMA KUU (MPAKA ALHAMISI MCHANA)

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu, umetupenda kupita kiasi
hata kumbebesha Mwanao mtiifu
makosa na maumivu yetu yote
tupate neema ya upatanisho:
ubariki basi jumuia hii inayotaka kula kidugu
ili ifanye daima mapenzi yako
yawe ndiyo chakula chake.
Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## TOKA ALHAMISI KUU JIONI HADI JUMAMOSI KUU

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Bwana Yesu Kristo,
ulishikamana kabisa na matakwa ya Baba yako
na kumtii mpaka kufa kwa ajili yetu.
Utubariki basi jamaa zako
tuliokusanyika mezani hapa;
tukijilisha chakula chako mwenyewe
tutambue jinsi mapenzi ya Mungu Baba
yalivyo mema, matamu tena makamilifu.
Unayeishi na kutawala daima na milele.**

## PASAKA - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu, ndiwe chanzo cha neema zote;
katika ufufuko wa Mwanao
umetuhamishia sisi pia kwenye uzima
kutoka hali ya mauti.
Sasa utubariki sisi na chakula hiki
ili hayo tunayoyaungama kwa imani
tuyashuhudie kwa matendo.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## PASAKA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Bwana Yesu Kristo, mfufuka kutoka wafu,
ulijitambulisha kwa wanafunzi wako
ulipowamegea mkate.
Tunaopokea sasa zawadi zako hizi
katika furaha angavu ya Pasaka,
tukukaribishe katika ndugu zetu
ili kweli ukae nasi Bwana.
Unayeishi na kutawala daima na milele.**

## PASAKA - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Tunakusifu, Baba, kwa ajili ya Yesu Kristo:
baada ya kuteswa aliwatokea wanafunzi wake
katika kumega mkate;
basi, kwa kutubariki sisi na neema hizi,
utujalie tumtambue Mwanao katika ndugu wote
tukastahili kula pamoja naye kwenye ufalme wako.
Anakoishi na kutawala daima na milele.**

## PASAKA - IV (KATI YA KUPAA BWANA NA PENTEKOSTE)

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba wa upendo, tunakushukuru
kwa kutumiminia moyoni Roho wa Mwanao
na kwa neema hizi tutakazoshirikiana;
ututendee tena maajabu ya zamani
na kuzidisha umoja tulionao.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## BIKIRA MARIA - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba yetu mwema,
katika Bikira Maria umelionyesha Kanisa lako
hali utakayolijalia mbinguni;
sisi tunamshangilia leo huyo
aliyebarikiwa kuliko wanawake wote
na pamoja tunakuomba
utubariki sisi pia na chakula hiki
ili maisha yetu yalingane na ya kwake
kwa utiifu na upendo.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## BIKIRA MARIA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu, kwa imani ya Mama yake
Yesu Mwanao alifanya arusi ya Kana isikose divai;
basi, kwa maombezi ya Bikira Maria
ubariki chakula chetu sisi watumishi wako
ukazuie neno lolote lisivuruge umoja wetu wa kidugu
wala mtu yeyote asikose riziki zake.
Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## WATAKATIFU

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu,**
**kwa wema wako uliwajalia watu**
**kuona maisha ya Kiinjili katika ndugu yetu F.**
**Sasa, kwa kutubarikia chakula hiki,**
**utuwashie ari ya watakatifu**
**waliotutangulia kufuata nyayo za Yesu**
**(mpole, mnyenyekevu aliyesulubiwa)**
**(*au*: safi, fukara na mtiifu).**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

## MTAKATIFU SOMO WA NDUGU FULANI

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba, unayetujalia furaha sisi wanao,**
**uitazame familia yako hii inayomshangilia leo ndugu F.**
**katika sikukuu ya somo wake.**
**Uibariki meza hii, ishara ya ushirika wetu,**
**na kwa maombezi ya mtakatifu F.**
**utujalie majina yetu yawe yameandikwa mbinguni.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KUTIMIZA MIAKA

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba, unayetujalia furaha sisi wanao,**
**uitazame familia yako hii inayomshangilia leo ndugu F.**
**kwa kutimiza miaka... tangu...**
**Uibariki meza hii, ishara ya ushirika wetu,**
**na katika safari yetu ya kila siku**
**utujalie tuonje zaidi na zaidi tunu ya udugu**
**na nguvu ya umoja wa kirafiki.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## AKIWEPO MGENI - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Wewe, Mungu, unawatembelea watu mfululizo.**
**Basi, utubariki sisi tunaompokea mgeni wetu F.**
**tukishirikiana naye kwa furaha mezani hapa.**
**Ushirika wetu wa kidugu ustawi siku kwa siku,**
**na macho yetu yazidi kuwa safi**
**ili katika sura ya ndugu zetu**
**tumtambue daima Mwanao,**
**anayeishi na kutawala daima na milele.**

## AKIWEPO MGENI - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba wa upendo na wema,**
**kwa Mwanao kujifanya mgeni wa akina Lazaro,**
**ulitakasa urafiki wa kibinadamu**
**uwe furaha ya moyo na faraja katika safari.**
**Tunakusifu kwa chakula tutakachoshirikiana**
**katika meza hii ya kidugu.**
**Pia tunaomba urafiki wetu**
**udumu kuwa mnyofu mpaka moyoni**
**kwa utukufu wa jina lako na utakatifu wa roho zetu.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## NAFASI YA FURAHA

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Ee Mungu, chemchemi ya furaha zote,**
**unatushirikisha maajabu yako kwa njia ya Mwanao:**
**tunakutukuza kwa zawadi hizi za upendo wako**
**na leo hasa kwa...**
**Ugeuze furaha ya siku hii**
**iwe heri ya milele mbinguni.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## MAFUNGO AU MAZOEZI YA KIROHO

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Wewe, Mungu, huonekani wala hueleweki:**
**ulipotaka kusema na moyo wa taifa lako**
**uliliongoza mpaka jangwani;**
**na ulipotaka kujifunua kwa watumishi wako**
**uliwaita wapande mlima mtakatifu.**
**Licha kutubarikia chakula tutakachoshirikiana**
**utufunulie leo (*au:* siku hizi) siri za upendo wako**
**na kutuonyesha utukufu wa uso wako.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KUKABIDHIWA HUDUMA AU DARAJA TAKATIFU

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Ee Mungu, uliikabidhi midomo yetu utangazaji wa Injili**
**na mikono yetu kazi ya wokovu wa watu;**
**basi, uipokee shukrani tunayokutolea**
**kwa mtumishi wako F. ambaye leo amekabidhiwa ...**
**Tena utubarikie kazi yake na chakula hiki.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KUPIGA HATUA UTAWANI

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mwenyezi Mungu,**
**nia yoyote njema ni neema yako tu:**
**baada ya kutufanya wanao kwa ubatizo**
**umetuita tumfuate Yesu katika jamaa yako hii.**
**Ubariki sasa chakula chetu cha kidugu**
**na kumjalia F. ambaye leo ameingia ... (*au*: ameweka...)**
**ayashuhudie pamoja nasi maisha ya Kiinjili**
**kwa kuitazama daima mifano ya Bikira Maria**
**mwenye moyo usio na doa.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## UCHAGUZI

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Utuangalie kwa upendo, Baba,**
**sisi tuliokusanyika ili tule pamoja:**
**udugu tunaoufurahia sasa**
**uwe mwongozo na mwanga kwa wale utakaowaweka (*au*: uliowaweka leo) kutuongoza.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu**.

## MIKUTANO MINGINE

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Baba mtakatifu sana,**
**kwa njia ya Bikira Maria, mtumishi wako mwaminifu,**
**umetupatia Yesu, kaka na rafiki bora:**
**tunakuomba ubariki chakula hiki**
**na bidii zetu za kutengeneza upya maisha yetu**
**ili tufuate nyayo zake.**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

## SIKU YA UDUGU WETU

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Kweli unatupenda, Baba!**
**Tunakusifu kwa paji la Roho Mtakatifu**
**ulilowajalia wafuasi wa Mwanao**
**wanaodumu kusali pamoja na Bikira Maria;**
**vilevile tunakushukuru kwa chakula**
**unachotushirikisha katika siku hii ya udugu wetu;**
**kitusaidie kuimarisha urafiki wetu**
**na kuitengeneza upya mioyo yetu.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## SHIDA ZA JAMII

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Mungu wa huruma,**
**ulitaka Yesu Mwanao awe sawa na mtu yeyote**
**na kujua uchungu ni nini;**
**ubariki chakula tunachokikaribia pamoja,**
**tena utufumbue macho na mioyo**
**tuwe na huruma na upendo kwa wenzetu**
**waliopata msiba wa ...**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KIFO

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa sala rasmi:

**Faraja zote zinatoka kwako, Mungu,**
**ambaye umeshinda kifo chetu kwa kifo cha Mwanao**
**na kutujalia uzima kwa ufufuko wake.**
**Utubariki sisi na chochote tutakachokula hivi punde:**
**tena ndugu F. ambaye hashiriki tena chakula chetu,**
**umkaribishe katika karamu yako mbinguni,**
**ambayo sisi pia tunatumaini utatushirikisha.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## SIKU YOYOTE

Mwanzoni wote wanajifanyia ishara ya msalaba, halafu kiongozi anasali hivi:

**Utubariki, Mungu wetu, sisi na chakula chetu,**
**tupate nguvu za kukutumikia vema.**

*Au:* **Utubariki, Baba, sisi na zawadi zako hizi**
**tunazozipokea kwa mikono miwili**
**kama ishara ya wema wako.**

*Au:* **Utujalie ulinzi wako, ee Bwana,**
**na kutegemeza udhaifu wetu**
**kwa chakula hiki ulichotuandalia.**

*Au:* **Zawadi zako hizi, Bwana, zituburudishe,**
**na neema zako zitufariji.**

*Au:* **Kila kilicho chema chatoka kwako, Baba wa nuru:**
**utubarikie sisi na chakula hiki,**
**tunachotaka kukipokea kwa shukrani.**

*Au:* **Usifiwe Baba Mwenyezi**
**unayetujalia mkate wetu wa kila siku.**
**Asifiwe Mwanao wa pekee**
**anayetulisha kwa neno lake.**
**Asifiwe Roho wako Mtakatifu**
**anayetuunganisha katika udugu mezani hapa.**

*Au:* **Baba, chemchemi ya mema yote,**
**utubariki sisi na chakula hiki**
**ili tuwe kitu kimoja ndani mwako**
**na kuishi kidugu kweli.**

Wote wanaitikia:
**Amina.**

# BAADA YA KULA

KAWAIDA - I

Kiongozi anaimba au kusema:
**Mbingu ni zako, ee Bwana, na nchi ni yako...**

Wote wanaitikia:
**... ndiwe uliyeumba ulimwengu na kila kitu kilichomo.**

Kiongozi anaalika wote wasali:
**Tuombe.**

Baada ya kimya, kiongozi anamalizia kwa sala rasmi:
**Tunakushukuru, Mungu, kwa maongozi yako:**
**wewe uliyetulisha kwa zawadi za leo**
**utujalie bidii mpya rohoni**
**pamoja na nguvu mwilini.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

Wote wanaitikia:
**Amina.**

Kiongozi akipenda anaweza kuongeza:
**Uwajalie watu wote chakula wanachohitaji**
**ili waungane nasi katika kukushukuru.**

*Au:* **Mtu yeyote asikose kamwe chakula, uhuru na amani,**
**ili tukushukuru sote pamoja.**

*Au:* **Uwalipe waliotusaidia kwa upendo wako**
**na uwajalie uzima wa milele.**

*Au:* **Uwarudishie wafadhili wetu**
**mara mia zaidi duniani hapa**
**na furaha ya milele katika ufalme wako.**

Wote wanaitikia:
**Amina.**

KAWAIDA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Tazama, tazama, ni vema na vizuri...**

W. **... ndugu kuishi pamoja kwa umoja.**

K. **Mema yote tunayapata kwako, Bwana,**
**uliyepanga watumishi wako wasikose mahitaji yao.**
**Tunatoa shukrani na kukuomba:**
**uwabariki wafadhili wetu**
**na kutujalia sisi pia**
**tugawane chakula na wenzetu.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mbingu ni zako, ee Bwana, na nchi ni yako...**

W. **... ndiwe uliyeumba ulimwengu na kila kitu kilichomo.**

K. **Tunakushukuru, Baba mtakatifu sana:
kisha kutujalia chakula kwa njaa yetu
na kinywaji kwa kiu yetu,
utushirikishe milele katika karamu yako
na katika wimbo wa sifa zako.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - IV

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Nitamhimidi Bwana kila wakati...**

W. **... sifa zake zi kinywani mwangu daima.**

K. **Baba, umetulisha kwa wingi wa neema zako:
utushibishe hasa kwa upendo wako
katika Kristo Mwanao,
anayeishi na kutawala daima na milele.**

## KAWAIDA - V

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Ndiwe uliyeumba ulimwengu...**

W. **... na kila kitu kilichomo.**

K. **Tunakushukuru, Mungu wetu
kwa neema yako tuliyoshiriki kidugu:
iimarishe umoja wetu nawe,
umoja kati yetu,
tena na viumbe vyote.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - VI

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Ndiwe uliyeumba ulimwengu...**

W. **... na kila kitu kilichomo.**

K. **Tunakushukuru Baba yetu
kwa chakula ulichotushirikisha wanao;
utujalie nasi tushirikishane vipaji na neema
tukaketi pamoja mezani pako milele.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

KAWAIDA - VII

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Tukipenda wenzetu...**

W. **...kati yetu Mungu yupo.**

K. **Ee Bwana, unayemlisha kila mwenye uhai,
utulinde katika upendo wako
sisi tuliogawana chakula kimoja,
tena utufanye tuwashughulikie kwa moyo
walio wadogo hasa
kwa kushirikiana nao katika riziki za dunia hii
na katika utajiri wa ufalme wako.
Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

KAWAIDA - VIII

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Tukipenda wenzetu...**

W. **... kati yetu Mungu yupo.**

K. **Tunakushukuru, Baba mwema:
chakula ulichotujalia mezani hapa
kichangie maendeleo yetu ya kiroho pia.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

KAWAIDA - IX

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Tazama, tazama, ni vema na vizuri...**

W. **... ndugu kuishi pamoja kwa umoja.**

K. **Mwenyezi Mungu, chakula tulichogawana
kitusaidie kuishi:
kwa neema yako utujalie tushibishe wenye njaa
na kuwasha mioyoni pia upendo halisi unaotoka
kwako
na ambao kwao tunarudi kwako.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

KAWAIDA - X

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Msifuni Bwana, viumbe, msifuni Bwana...**

W. **... msifuni Bwana, viumbe, msifuni Bwana.**

K. **Baba yetu mwema, mpaji wa mema yote,
tunakushukuru kwa kutukusanya leo chakulani;
kwa nguvu mpya ulizotujalia mwilini
tuendelee kwa bidii safari yetu ya hapa duniani
tukafike salama salimini kwenye karamu ya
mbinguni.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KAWAIDA - XI

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Nitamhimidi Bwana kila wakati...**

W. **... sifa zake zi kinywani mwangu daima.**

K. **Kwa jina lako, Bwana,**
**tumekusanyika na kuburudika mezani;**
**basi tunakushukuru kwa neema hizo**
**na kukuomba roho zetu pia ziimarishwe nawe**
**tuweze kumfuata Kristo kwa matendo na ukweli.**
**Yeye anayeishi na kutawala daima na milele.**

## KAWAIDA - XII

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Msifuni Bwana, viumbe, msifuni Bwana...**

W. **... msifuni Bwana, viumbe, msifuni Bwana.**

K. **Baada ya kula pamoja, Bwana,**
**tunakushukuru pamoja:**
**maisha yetu ya kidugu yaonyeshe wazi umoja**
**unaopatikana katika Yesu na katika Kanisa lake.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## MAJILIO - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kesheni kila wakati, ndugu, kila wakati...**

W. **... mpate kuokoka.**

K. **Mungu wa upendo, unayemiliki nyakati zote,**
**tunakushukuru kwa misaada hii ya kujengea miili,**
**ambayo tunakuomba isifanye nzito roho zetu.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## MAJILIO - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kesheni kila wakati, ndugu, kila wakati...**

W. **... mpate kuokoka.**

K. **Asante, Baba mwema,**
**kwa kutukusanya wanao**
**kwenye meza hii ya kidugu;**
**uzidi kutukeshea sisi sote,**
**kusudi kwa roho nyepesi na ya furaha**
**tuendelee kutafuta kwanza ufalme wako.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

MAJILIO - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Tafuteni kwanza ufalme wa mbingu…**

W. **… mengine yote mtapewa kwa ziada.**

K. **Asante, Baba, kwa chakula**
**tulichojaliwa na ukarimu wako mkuu.**
**Uwabariki wanaotuwezesha kufanya kazi zetu,**
**na utujalie sisi, tuliopata kwanza nguvu,**
**tukamlaki Mwanao**
**kwa matendo ya imani, haki na upendo halisi.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

MAJILIO - IV

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Tafuteni kwanza ufalme wa mbingu…**

W. **… mengine yote mtapewa kwa ziada.**

K. **Kwa nguvu ya chakula cha leo, Bwana,**
**utujalie sisi tuwe sauti na mwanga**
**ili wengine wengi wajiandae kukutana nawe.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

NOELI - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Neno alifanyika mwili…**

W. **… nasi tukauona utukufu wake.**

K. **Tunakushukuru, Baba mtakatifu sana,**
**uliyemtuma Neno wako**
**ashiriki ubinadamu wetu**
**na kujifanya chakula chetu.**
**Utudumishe katika utumishi wako**
**tuweze kuwa chombo cha maongozi yako**
**kwa mafukara wa ulimwengu huu.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

NOELI - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mwokozi kazaliwa, tuimbe aleluya…**

W. **… Mwokozi kazaliwa, aleluya.**

K. **Asante, Baba, kwa neema zako tulizopokea kwanza,**
**na asante zaidi kwa kutupatia Kristo Mwanao**
**aliye Mkate, Neno, Rafiki na Kiongozi**
**kwenye njia nyembamba inayofika kwako.**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

## KWARESIMA - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mtu hataishi kwa mkate tu...**

W. **... ila kwa kila neno litokalo katika kinywa chake Mungu.**

K. **Katika mfungo wa Mwanao, ee Baba,
umetufundisha kuwa njaa ya binadamu
haiwezi kutulizwa na chakula cha mwili
pasipo neno la uzima.
Utusaidie tusijipendee kamwe,
bali tuwe tayari daima kushirikishana na wenzetu,
kusudi ifutwe njaa yoyote ya roho na ya mwili.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KWARESIMA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mtu hataishi kwa mkate tu...**

W. **... ila kwa kila neno litokalo katika kinywa chake Mungu.**

K. **Tunapozidi kuitiisha miili yetu kwako, Baba,
utusaidie kukuinulia mioyo yetu
na kujiandaa tuonje kwa roho mpya
furaha ya Pasaka pamoja na wenzetu.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KWARESIMA - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mimi mwenyewe nitawalisha kondoo zangu...**

W. **... nami nitawalaza, asema Bwana.**

K. **Uwezo wote ni wako, Baba,
uliyetuumba kwa hekima ya ajabu
na kutuchunga mpaka leo.
Pokea sala yetu ya shukrani
na kuongoza hatua zetu kwenye njia za toba,
yaani kusali, kujinyima na kupendana,
ili tulitimize neno lako na kuishi kwa haki.
Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## KWARESIMA - IV

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mimi mwenyewe nitawalisha kondoo zangu...**

W. **... nami nitawalaza, asema Bwana.**

K. **Tunakushukuru, Bwana, kwa chakula hiki
na kukuomba dhamiri zetu zisitulie kwa siku moja tu
ya kujinyima chakula na kugawana na wenzetu,
bali tuendelee kuyatambua matatizo ya watu
na kujenga haki duniani;
tena tumshuhudie Yesu mwema kwa matendo ya upendo
ili wote wampokee mioyoni mwao yeye,
anayeishi na kutawala daima na milele.**

## JUMA KUU

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kristo amekuwa mtii kwa ajili yetu...**

W. **... mpaka kufa, hata kufa msalabani, hata kufa msalabani.**

K. **Baba wa mataifa yote,**
**tunakushukuru tena kwa upendo wako**
**usio na mipaka wala gharama kwetu:**
**neema ya udugu tuliyopokea mezani**
**itusaidie kutumikia maishani.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

## PASAKA - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kristo, Paska yetu, amechinjwa sadaka...**

W. **... tuile karamuye na tuimbe aleluya.**

K. **Ee Mungu, chemchemi ya uzima,**
**kisha kutujalia chakula kwa maisha ya hapa duniani,**
**utujaze mioyo furaha ya Pasaka**
**na kutudumisha katika uzima mpya**
**alioanzisha ndani mwetu Yesu Kristo mfufuka.**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

## PASAKA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kristo, Paska yetu, amechinjwa sadaka...**

W. **... tuile karamuye na tuimbe aleluya.**

K. **Tunakushukuru, Baba, kwa neema zako zote:**
**utushirikishe hasa katika karamu ile ambayo**
**Bwana mfufuka amestahili na kuandaa kwa ajili yetu.**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

## PASAKA - III

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kristo, Kristo, Pasaka yetu, amejitoa sadaka...**

W. **... tuile, tuile karamuye na tuimbe aleluya.**

K. **Hata leo, Bwana, umetujalia nguvu mpya:**
**tuzitumie kwa kutengeneza maisha yetu**
**yalingane daima na uzima mpya**
**aliotupatia Mwanao mfufuka,**
**yaweze kuonyesha shukrani tuliyonayo moyoni.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

PASAKA - IV

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kristo, Kristo, Pasaka yetu, amejitoa sadaka...**

W. **... tuile, tuile karamuye na tuimbe aleluya.**

K. **Muumba wa watu wote,**
**utuangalie kwa wema sisi familia yako**
**tulioketi kula pamoja hapa duniani,**
**ukatujalie sisi na mataifa yote**
**tushiriki milele katika karamu ya arusi**
**ya Mwanakondoo aliyechinjwa.**
**Anayeishi na kutawala daima na milele.**

PASAKA - V (KATI YA KUPAA BWANA NA PENTEKOSTE)

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kukaja upepo kutoka mbinguni juu...**

W. **... na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, ale, aleluya, ale, aleluya.**

K. **Mungu, Baba yetu sote,**
**ututazame kwa upendo wanao tuliokusanyika mezani:**
**upendo huo uliotushirikisha hapa**
**ukamilishwe na Roho wako uwe heri ya Pasaka ya milele.**
**Kwa njia ya Kristo, Bwana wetu.**

PASAKA - VI (KATI YA KUPAA BWANA NA PENTEKOSTE)

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Kukaja upepo kutoka mbinguni juu...**

W. **... na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, ale, aleluya, ale, aleluya.**

K. **Asante, Bwana, kwa neema zako hizi.**
**Sasa tunakuomba sana:**
**utushushie Roho wako wa upendo**
**ili sisi uliotushibisha kwa chakula kimoja**
**tuendelee kuwa kitu kimoja ndani yako.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

BIKIRA MARIA - I

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mimi ni mtumishi wake Bwana...**

W. **... nitendewe ulivyonena.**

K. **Tunakushukuru, Mungu Baba,**
**kwa kutujalia siku zote chakula cha duniani,**
**wewe mwenyewe ambaye kwa njia ya Maria,**
**mtumishi wako mwaminifu,**
**umetujalia Mkate kutoka mbinguni,**
**Yesu Kristo Mwanao,**
**anayeishi na kutawala daima na milele.**

BIKIRA MARIA - II

Yote ni kama hapo juu, isipokuwa:

K. **Mimi ni mtumishi wake Bwana...**

W. **... nitendewe ulivyonena.**

K. **Ee Mungu, Bwana wetu,**
**ulimwangalia kwa huruma mjakazi wako mnyenyekevu**
**ukawashibisha mema wenye njaa;**
**kwa mfano wa Bikira Maria**
**tunakushukuru kwa neema tulizopokea**
**sisi tunaokutegemea wewe tu,**
**tukiamini kabisa hatutapungukiwa kitu.**
**Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**